**CHATO COLLEGE OF HEALTH SCIENCES AND TECHNOLOGY**

P.O. Box 73, Chato – Geita – Tanzania

Tel: +255 784 638 495 / +255 767 150 048 / +255 763 759 363/ +255 746 154 600

**Website:www.chatocollege.ac.tz: email: chatocohest@gmail.com**


**Kumb.Na:HAS.158/05/2024** **Tarehe: 01/04/2024**

**KWA NDUGU:**

………………………………………………………………………………………………………………………………………………

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO KATIKA CHUO CHA SAYANSI ZA AFYA NA TEKNOLOJIA-CHATO**

Napenda kutumia nafasi hii kukupongeza na kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na mafunzo katika Chuo cha Sayansi Za Afya na Teknolojia-chato kilichopo Mkoa wa Geita, Wilaya ya Chato katika kozi ya Stashahada ya utabibu **(Ordinary Diploma in Clinical Medicine)** kwa muda wa miaka **mitatu** kwa mwaka wa masomo **2024/2025.**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA KWA MWAKA WA MASOMO 2024/2025

### 1. MAELEKEZO YA JUMLA

1.1 **MAHALI:** Chuo kipo eneo la Mbuye katika kata ya Bwina chato mjini wilaya ya Chato Mkoa wa Geita.

1.2 Unapaswa kuripoti chuo cha sayansi za afya na teknolojia chato kati ya tarehe **02/09/2024** na tarehe **06/09/2024** ambapo masomo yataanza, kwa kuongozwa ipasavyo na ofisi ya udahili.

1.3 Nakala ya cheti cha kuhitimu kidato cha nne/sita na nakala ya cheti cha kuzaliwa kwa uhakiki .

1.4 Vifaa vya kutosha vya kujifunzia kama vile Daftari (counter books) kalamu, rula n.k

1.5 Mwamvuli au koti kwa ajili ya matumizi wakati wa majira ya mvua au baridi ili kuepusha kutohudhuria vipindi kwa sababu ya mvua (Hii ni hiari na si lazima).

1.6 Nguo na viatu vya michezo.

1.7 Taarifa ya kupima Afya (medical examination) kutoka kwenye hospital au kituo cha Afya

kinachotambulika.(Fomu imeambatanishwa na inapatikana kupitia **www.chatocollege.ac.tz**)

1.8 Vitendea kazi wakati wa mafunzo kwa vitendo –Blood pressure machine,Stethoscope,Clinical thermometer, Glucometer, Patella hammer,Foetoscope na clinical torch,unaweza ukaagiziwa kupitia chuo kwa gharama kuanzia Tshs 150,000 hadi 200,000/= vyote kwa pamoja kutegemea na aina ya kifaa au fika kwenye maduka ya vifaa vya maabara na hospitali).

1.9 Mwanafunzi aje na sweta lenye rangi nyeupe lisilo na nembo wala mandishi (plain) kwa ajili ya kujikinga na baridi

1.10 Rimu Tatu (3) za karatasi aina ya **Double A tu**,na si aina nyingine, mara tu anapofika chuoni hii ni kwa ajiri ya mitihani ya kila mwezi pamoja na ile ya kumaliza muhula.( hizi zitakuwa kwa kila mwaka)

1.11 Mfagio wa ndani ( Soft bloom) mmoja,Mfagio wa kudekia na ndoo yake (Mopper) moja,Pamoja na Leki ya kukusanyia takataka kwa ajili ya usafi wa mazingira.

## 2. UTARATIBU WA MALIPO YA ADA NA MICHANGO MINGINE YA CHUO ISIYOKUWA ADA

1. Malipo ya Ada pamoja na michango mingine ya Chuo yatafanyika kwa kutumia namba ya malipo (**CONTROL NUMBER**) Ambayo mwanafunzi atapatiwa baada ya kupiga simu namba hizi, **0763759363/0767150048/0767638495**
2. Malipo ya umoja wa wanafunzi shilingi **20,000** yafanyike kupitia Benki ya **NMB** akaunti Namba **32710021476** Jina la akaunti ni **CHATO COLLEGE OF HEALTH STUDENT'S ORGANIZATION**
   **na stakabadhi ya banki iwasilishwe kwa mhasibu wa chuo.**
3. Malipo ya Mitihani ya Taifa yatalipwa kila muhula wa pili wa masomo ambayo ni TSHS **150,000/=** kwa mwaka kwa wanafunzi wa kozi za Afya tu ambayo italipwa moja kwa moja wizara ya Afya fedha hizi mwanafunzi aje nazo moja kwa moja chuoni ili kupatiwa control namba ya malipo ya serikali kwa wanafunzi wote,(**ikumbukwe kuwa fedha hizi zikishalipwa hazitarudishwa kwa sababu yoyote ile)**.
4. ***KUMBUKA kutochanganya malipo haya pamoja na malipo ya Ada ya Chuo. (malipo ya ADA piga simu kama ilivyoelekezwa hapo juu)***

3. **MAHITAJI KWA AJILI HOSTELI.**

Yafuatayo ni mahitaji ambayo wanachuo wanapaswa kuja nayo kwa ajili ya Hosteli;-

- Shuka 4, Blanketi 1, chandarua cha pembe nne kinachoenea kwenye kitanda cha futi 3x6, foronya 1 na taulo 1.
- Ndoo moja ya plastic ya lita 20,ndoo moja ya lita 10 na Sanduku au Begi la kutunzia vitu vya thamani lenye kufungwa na kufuri kwa ajiri ya usalama binafsi.
- Godoro aina ya comfy au super banco la futi $2^{1}/_{2}$ kwa 6 kwa wanafunzi wote.

4. **SARE:**

Sare kwa wanafunzi wote watatakiwa kuwa na sare kwa mujibu wa miongozo ya Wizara ya Afya ambazo ni Gauni mbili (2) nyeupe kwa wasichana, suruali mbili (2) za khaki na mashati mawili meupe yenye mikono mifupi kwa wavulana, koti moja jeupe kwa ajili ya mazoezi kwa vitendo zinazopatikana kwa gharama ya Tshs 80,000/= fedha hii ilipwe chuoni wakati wa kuripoti.

**N.B:** Mwanafunzi aje na viatu vya ngozi vyenye rangi nyeusi kwa jinsia zote, Pia soksi nyeupe kwa wanawake, na soksi nyeusi au nyeupe kwa wanaume, pia aje na track suit nyeusi yenye mistari myeupe mikononi na sweta jeupe la darasani lisilokuwa na maandishi au nembo yoyote.

**KARIBU CHUONI**



*Dr Joel Limbu.Maduhu(MD,MPH,DCM).*

**MKUU WA CHUO**

# Chato College of Health Science and Technology.

## MUUNDO WA ADA NA MICHANGO MINGINE

**1. FEDHA INAYOLIPWA CHUO A. ADA YA MASOMO (TSHs)**

| **S/N** | **Maelezo** | **Kiasi (Tshs)** |
|---|---|---|
| a) | Ada ya mafunzo | 1,800,000/= |
| b) | Gharama na Michango Mingine | 565,000/= |
| | Jumla ya Ada ya masomo na Michango | 2,365,000/= |

### 1(b) MCHANGANUO WA GHARAMA NA MICHANGO MINGINE ZA CHUO(TSHs)

| SN | MAELEZO | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1 | Ada ya Usajili | 50,000 |
| 2 | Ukaguzi wa Udhibiti wa viwango vya ubora( NACTE QUALITY ASSURANCE FEE) | 15,000 |
| 3 | Ukarabati, Maji na Umeme | 100,000 |
| 4 | Gharama ya mitihani na majaribio ya ndani(Chuoni) | 100,000 |
| 5 | Maktaba, Maabara ya Komputa na Mtandao | 150,000 |
| 6 | Fedha ya tahadhari | 50,000 |
| 6 | Mazoezi ya vitendo na vitendanishi (practical & reagents) | 100,000 |
| | JUMLA KUU YA FEDHA | 565,000 |

**NB**;Malipo ya Ada pamoja na michango mingine ya Chuo yatafanyika kwa kutumia namba ya malipo (**CONTROL NUMBER**) Ambayo mwanafunzi atapatiwa baada ya kupiga simu namba hizi, **0763759363/0767150048/0767638495**

### 2. UMOJA WA WANAFUNZI NA BIMA YA AFYA (KWA WASIOKUWA NA BIMA)

| SN | Maelezo | Akaunti | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1 | Fedha ya umoja wa wanafunzi | **32710021476 (CHATO COLLEGE OF HEALTH STUDENT'S ORGANIZATION – NMB)** | 20, 000 |
| 2 | Bima ya Afya - NHIF (Kwa wanafunzi wasiokuwa na bima ya afya) | **284401000003 (Chato College of Health Sciences and Technology - TCB)** | 50,400/= |

**NB: Stakabadhi ya benki ya malipo tajwa hapo juu iwasilishwe kwa mhasibu wa chuo pale mwanafunzi anaporipoti chuoni. Wanafunzi wasiokuwa na namba ya Nida wanashauriwa kuwasiliana na ofisi ya Mfuko wa Bima ya Afya kabla ya kuripoti chuoni na kuwasilisha nakala ya kadi ya Bima ya afya wakati wa kuripoti**

3. **MCHANGANUO WA AWAMU ZA MALIPO IMEONYESHWA HAPA CHINI KWA ATAKAYEHITAJI KULIPA KWA AWAMU.**

| AINA YA MALIPO | AWAMU YA I September – December | AWAMU YA II (Jan-March) | AWAMU YA III (April-MAY) | AWAMU YA IV June - July | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| Ada ya Chuo (Pharmaceutical Sciences) | 450,000/= | 450,000/= | 450,000/= | 450,000/= | 1,800,000/= |
| Gharama na Michango mingine isiyo ada | 250,000/= | 200,000/= | 65,000/= | 50,000/= | 565,000/= |
| Chakula | 350,000/= | 200,000/= | 150,000/= | 100,000/= | 800,000/= |
| **Jumla (Bweni)** | **1,050,000/=** | **850,000/=** | **665,000/=** | **600,000/=** | **3,165,000/=** |
| **Jumla (Kutwa)** | **700,000/=** | **650,000/=** | **515,000/=** | **500,000/=** | **2,365,000/=** |

**NB; Kutakuwa na malipo pindi mwanafunzi atakapoenda field, fedha hizo zitakazomsaidia kujikimu kwa muda atakaotumia field kiasi cha Tsh 200,000/=, Ikumbukwe fedha hizi ni za kujikimu mwanafunzi pamoja na Kituo atakachopangiwa.**

Principal
Chato College Of Health Sciences
And Technology
P. O. Box 73, Chato, Geita - Tanzania

*Dr Joel Limbu.Maduhu(MD,MPH,DCM).*

**MKUU WA CHUO**

**Chato College of Health Science and Technology**